Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

SHULE YA SEKONDARI PANKUMBI

MTIHANI WA MWISHO WA MWAKA KIDATO CHA TATU

021 **KISWAHILI**

MUDA:SAA 2:30

MAELEKEZO

1 Mtihani huu una sehemu A,B na C.Jibu maswali yote katika sehemu A na B kisha maswali matatu katika sehemu C

2.Zingatia maagizo ya kila sehemu na kila swali

3 .Piga mistari ya pambizo katika kijitabu chako cha kujibia kila ukurasa pande zote nne(juu,chini,kulia na kushoto) kwa ukubwa wa rula

SEHEMU A (ALAMA 15

1.Chagua jibu sahihi zaidi miongoni mwa majibu uliyopewa;

i) Wahusika wa fasihi andishi kwa kigezo cha dhamira wanazoibua;

a) Wasika bapa,wahusika shinda,wahusika foili

b) Wahusika mviringo/duara,wahusika bapa,wahusika shinda /foili ( )

c) Wahusika wakuu,wahusika bapa,wahusika wajenzi

d) Wahusika wajenzi,wahusika wakuu,wahusika wasaidizi

ii) Mbinu ya kisanaa ambapo mtunzi hufululiza maneno mengi bila kuweka kiunganishi baina ya hayo maneno;

a) Tasfida

b) Tashihisi ( )

C) Takriri

d) Mjalizo

iii) Maneno yasiyosanifu yanayozuka na kutumika katika eneo dogo sana.Inaweza kuwa katika ofisi au taasisi Fulani tu;

a) Misimu ya kisasa

b) Misimu ya pekee ( )

c) Misimu ya kitarafa

d) Misimu zagao

iv) Lahaja za kusini;

a) Kimakunduchi,kiunguja,kipemba,kingazija,kinzwani

b) kinzwani,kimtang`ata,chimiini,kipate,kiungwana

c) kingao,kipate,kiamu,kingozi,Chichifundi ( )

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

d) kihadimu,kimafia,kimrima,kipate,kiunguja

v) Yule ***ni*** mlevi. ”ni” ni aina gani ya neno?;
a) kitenzi kikuu
b) kiunganishi
c) kitenzi kisaidizi ( )
d) kitenzi kishirikishi

vi) Utamkaji unaomtambulisha mtu asili yake;
a) Lafudhi
b) Mkazo ( )
c) Kiimbo
d) Lugha

vii) Vifuatavyo ni vigezo vya kiisimu vinavyothibitisha ubantu wa Kiswahili isipokuwa;
a) Ushairi wa Kiswahili
b) Msamiati
c) Muundo wa sentensi ( )
d) Upatanisho wa kisarufi

viii) O-YO ni O-rejeshi ya ngeli gani kati ya hizi?;
a) LI-YA
b) U-I ( )
c) KI-VI
d) PAMUKU

ix) ***Mazingara*** ya shule ni machafu;
a) Kosa la kimuundo
b) Kosa la kimatamshi ( )
c) kosa la kimsamiati
d) kosa la kuongeza vitamkwa

x) Taja seti iliyosahihi katika mambo yanayounda fasili ya lugha:
a) Sauti,nasibu,kukubaliwa na jamii,,maana,kufurahisha
b) Sauti,nasibu,maana,kukubaliwa na jamii,kukidhi haja ya mawasiliano ( )
c) Sauti,nasibu,maana,kukubaliwa na jamii,kuelimisha
d) Kukidhi haja ya mawasiliano,sauti,nasibu,maana,kukosoa jamii

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

2.Oanisha orodha A na B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi mbele ya maelezo ya orodha A

ORODHA A	ORODHA B
i) Tashihisi……	a) Kauli au neno linalopunguza ukali wa maneno
ii) Tashititi……..	b) Kuuliza swali ambalo majibu yake unayajua
iii) Takriri……	c) Vitu visivyobinadamu kupewa uwezo wa kutenda kama binadamu
iv) Tasfida…….	d) kulinganisha vitu kwa kutumia maneno ya ulinganisho
v) Tashibiha……..	e) kulinganisha vitu bila kutumia maneno ya ulinganisho
	f) Kutia chumvi maelezo
	g) kurudiarudia silabi,maneno au sentensi
	h) kupunguza ukali wa maneno

SEHEMU B (ALAMA 40)

3.Bainisha O-rejeshi za nomino zifuatazo;(onesha na mchakato uliotumia kuzipata hizo o-rejeshi)

i) Mkulima ii) Kibatari iii) Kunywa iv) Mkono

4.Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi/ ngoe

.*Baba yangu alikuwa analima shamba letu vizuri*

5.Eleza kwa kifupi maana ya dhana zifuatazo za kifasihi

i) Riwaya pendwa ii) Riwaya dhati iii) Tamthiliya Tanzia iv) Tamthiliya Ramsa

6.Utohoaji ni njia mojawapo ya uundaji wa maneno ya kiswahili kwa kulichukua neno kutoka lugha nyingine.Taja lugha ambako maneno yafuatayo yametoka;

i) Ngeli ii) Shamba iii) Rijari iv) Taulo v) Meza vi) Korosho vii) Tumbaku Viii) Ng`atuka

7.Taja njia iliyotumika kuunda misimu ifuatayo;

i) Mataputapu(pombe) ii) Kibamia (utupu wa mwanaume) iii) k (utupu wa mwanamke)
iv) Prezidaa(Rais)

8.Sarufi ni sheria na kanuni zinazomwongoza mtu kutumia lugha kwa ufasaha.Toa maelezo mafupi kuhusu aina nne za sarufi.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

SEHEMU C (ALAMA 45)

9.a) Kwa kutumia mchoro onesha muundo wa barua za magazetini

b) Chukulia kuwa wewe ni Papaa Zahera uishiye mtaa wa Iwambala jijini Mbeya.mwezi uliopita Halmashauri ya jiji ilirundika vifusi katika barabara za mtaani kwako lakini hadi leo vifusi hivyo havijasambazwa kiasi cha kuzifanya barabara hizo kutopitika kabisa kwa mwezi mzima.Andika barua kwa mhariri wa gazeti la *Tanzania Daima* kulalamikia kero hii.Anza na kichwa cha habari *JIJI LA MBEYA LISAMBAZE VIFUSI KATIKA BARABARA ZA MITAA*. Anuani yako ni SLP 2929 Mbeya

ORODHA YA VITABU TEULE KWA SWALI LA 10-12

USHAIRI

- WASAKATONGE -M.S Khatibu (Dup)
- MALENGO WAPYA -TAKILUKI (HP)
- MASHAIRI YA CHEKECHEKA -T.A. MVUNGI (EP & D.LTD)

RIWAYA

- TAKADINI Ben Hanson (MBS)
- WATOTO WA MAMA NTILIE E. mbogo (HP)
- JOKA LA MDIMU A.J Safari (HP)

TAMTHILIYA

- ORODHA Steven Reynold (MA)
- NGOSWE PENZI KITOVU CHA UZEMBE E. Semzaba ESC)
- KILIO CHETU Medical aid Foundation (APH)

10.Waandishi wa diwani siku zote huandika mambo yasiyo na uhalisia.Kanusha kauli hiyo kwa hoja tatu kutoka kwa kila malenga wawili.

11.Riwaya ya **Watoto Wa Mama N`tilie**,**Joka la Mdimu** na **Takadini** ni mfano bora wa riwaya dhati.Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa hoja tatu kutoka katika kila riwaya miongoni mwa riwaya mbili zilizotajwa hapo juu.

12.Katika jamii ya sasa kuna mambo mengi sana yasiyofaa ambayo hutendwa na wanajamii.Je,ni kwa vipi waandishi wa tamthiliya mbili ulizosoma wamejishughulisha kukemea mambo hayo yasiyofaa?.Toa hoja tatu kwa kila tamthiliya.Tumia vitabu viwili tu.

TAMATI

Search ⇢ www.africona.net